Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

---

326. **Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. katika** *Bihar al- Anwar , J. 74, Uk. 301:*

"Ni faradhi kwa kila Mwislamu kusitiri na kuzificha aibu sabini (70) za Mwislamu mwenzake (*ili kulinda heshima yake*)."

(Makosa na kasoro zake zote zishughulikiwe kibinafsi na wala zisienezwe na kutangazwa kwa watu wengine).

327. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.Amesema katika** *Bihar al- Anwar, J. 74, Uk. 165:*

"Kubali msamaha akuombao Nduguyo Mwislamu na kama hakufanya hivyo, jaribu kumvumbulia hivyo."

328. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.Amesema katika** *Mustadrak Al-Wasa'il al-Shiah'il-ush-Shiah, J. 12, Uk. 305 na 14155:*

"Hali mbaya kabisa ya uhaini ni kutoboa habari zilizo siri."

329. **Al Imam 'Ali ibn Abi Talib a.s.Amesema katika** *Ghurar-ul-Hikam, Uk. 322:*

"Kumuonya kwako aliyetenda makosa miongoni mwao au mbele ya watu ni kumdhalilisha." (Inakubidi uongee naye katika faragha)."

330. **Amesema Al-Imam Ja'far as-Sadiq a.s.katika** *Al-Kafi, J. 2, Uk. 192:*

"Katika matendo yote ayapendayo Allah swt, ni kule kumletea furaha Mwislamu kwa mfano: kumshibisha, kumwondolea majonzi yake, au kumlipia madeni yake."

Source URL:
https://www.al-islam.org/hadith-za-mtume-s-na-ma-imamu-amiraly-m-h-datoo/kulinda-heshima-ya-waumini